

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA SITA

KIKAO CHA TATU

03 FEBRUARI, 2022



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA SITA

KIKAO CHA TATU – TAREHE 03 FEBRUARI, 2022

I. DUA:

II. MASWALI:

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

16. **MHESHIMIWA HUSSEIN NASSOR AMAR
(NYANG’HWALE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza Watumishi katika Vituo vya Afya vya Kharumwa na Nyang’hwale.

WIZARA YA NISHATI:

17. MHESHIMIWA DKT. JOHN DANIELSON PALLANGYO (ARUMERU MASHARIKI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, ni lini Serikali itaunganisha umeme wa REA kwa Wananchi wa Vijiji vilivyopo katika Kata za Jimbo la Arumeru Mashariki ambazo hazina umeme.

18. MHESHIMIWA FLATEI GREGORY MASSAY (MBULU VIJIJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi yake ya kupeleka umeme katika Vijiji na Vitongoji vya Jimbo la Mbulu Vijijini.

WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:

19. MHESHIMIWA NEEMA KICHIKI LUGANGIRA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum:-

Je, Serikali haioni haja ya kuja na mpango mkakati wa kuwezesha NGO'S kupata rasilimali fedha kupitia njia mbalimbali ikiwemo ruzuku katika maeneo mahsusi kama ambavyo inafanyika kwa Vyama vya Siasa hasa baada ya uamuzi wa Serikali kuanzisha Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum ambayo inahusisha Asasi za Kiraia katika malengo yake.

WIZARA YA KILIMO:

20. MHESHIMIWA MIRAJI JUMANNE MTATURU (SINGIDA MASHARIKI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kukamilisha ujenzi wa Skimu ya Umwagiliaji Mang'onyi ili kuongeza tija ya kilimo cha Mbogamboga kwenye Kata za Mang'onyi na Makiungu.

21. MHESHIMIWA SHALLY JOSEPHA RAYMOND (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, ni Mikoa ipi inaongoza kwa mafanikio katika kampeni ya kuwabadili Wakulima kutoka kwenye kilimo cha kujikimu na kulima kibiashara na ni Mikoa ipi bado inasuasua.

WIZARA YA MAJI:

22. MHESHIMIWA CONDESTER MICHAEL SICHALWE (MOMBA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, ni lini Serikali itatatua changamoto ya maji katika Jimbo la Momba.



23. MHESHIMIWA ANATROPIA LWEHIKILA THEONEST (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, ni lini Serikali itawapatia maji Wananchi wa Wilaya ya Kyerwa kwa kutengeneza miundombinu ya kupeleka maji kwa Wakazi waishio sehemu za miinuko.

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

24. MHESHIMIWA STELLA IKUPA ALEX (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuingiza lugha ya alama kwenye Mitaala ya Elimu nchini.

25. MHESHIMIWA DKT. OSCAR ISHENGOMA KIKOYO (MULEBA KUSINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:-

Je, Serikali ina mkakati gani mahsusi wa kuhakikisha Vijana wote wanaoomba mikopo ya Elimu ya Juu wanapata mikopo hiyo kama walivyoomba.

III. MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI:

(Kusomwa Mara ya Kwanza)

Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Kudhibiti Utakatishaji wa Fedha Haramu wa Mwaka 2022 (*The Anti – Money Laundering (Amendment) Bill, 2022*).



DODOMA
03 FEBRUARI, 2022

N.J. MWIHAMBI, *ndc*
KATIBU WA BUNGE

